WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Baraza la Kiswahili la Taifa
BAKITA

UNESCO

# MWONGOZO WA KONGAMANO LA PILI LA KISWAHILI LA KIMATAIFA

## PARIS, UFARANSA | 4-7 Julai 2026




"Kiswahili kwa Amani, Mshikamano na Diplomasia ya Uchumi Duniani"

# MWONGOZO WA KONGAMANO LA PILI LA KISWAHILI LA KIMATAIFA

## PARIS, UFARANSA

## Tarehe 4-7 Julai 2026

**"Kiswahili kwa Amani, Mshikamano na Diplomasia ya Uchumi Duniani"**

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



"Kiswahili si tu lugha ya mawasiliano, bali ni nyenzo muhimu ya diplomasia, utamaduni, na mtangamano inayounganisha watu wetu na kuchochea Maendeleo Endelevu katika ukanda wetu."

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



# Yaliyomo

**Nukuu ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania........................................ii**

**Yaliyomo**.....................................................................................iii

**Ujumbe wa Waziri**.........................................................................vi

**Dibaji**.........................................................................................viii

**Salamu za Ukaribisho**......................................................................x

**SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA**..................... 1

**Usuli wa Kongamano**.............................................................. 1

**Malengo ya Kongamano**.......................................................... 3

**Lengo Kuu**............................................................................... 3

**Malengo Mahsusi**.................................................................... 3

**Matokeo ya Kongamano la Kwanza**........................................ 4

**Washiriki wa Kongamano la Pili**............................................. 5

**SEHEMU YA PILI: MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA**....... 9

**Usajili**...................................................................................... 9

**Mahitaji ya Viza**...................................................................... 9

**Bima ya Safari**........................................................................ 10

**Chanjo na Huduma za Afya**.................................................... 10

**Gharama za Usafiri na Malazi**................................................. 11

**Gharama za Mashirika Mbalimbali ya Ndege**.......................... 11

**Utaratibu wa Safari ya Kwenda kwenye Kongamano**.............. 12

**Hali ya Hewa............................................ .,.........................................14**

Utaratibu wa Mavazi Wakati wa Kongamano .................................. 14

Mkakati wa Mawasiliano ............................................................ 14

Njia za Mawasiliano Nchini Ufaransa ............................................ 15

Mawasiliano kuhusu Kongamano ................................................. 15

SEHEMU YA TATU: MATUKIO YA KONGAMANO ..................... 17

Ufunguzi wa Kongamano ............................................................ 17

Ziara ........................................................................................ 17

Uwasilishaji wa Makala za Kitaaluma .......................................... 19

Tamasha la Kiswahili ................................................................ 23

Maonesho Mbalimbali ................................................................ 24

Burudani .................................................................................. 26

Vikao vya Miadi na *Tete-a-tete* ................................................... 27

Uzinduzi wa Machapisho ........................................................... 28

Utiaji Saini wa Hati za Makubaliano na Ushirikiano .................. 29

Utoaji wa Tuzo .......................................................................... 30

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani ............... 30

SEHEMU YA NNE: HITIMISHO .................................................. 31

Wito kwa Washiriki .................................................................... 31

2027 Tanzania Haitapoa: Karibuni kwa AFCON na *Miss World* 32

VIAMBATISHO .......................................................................... 33

A. Mwongozo wa Kupata Viza..................... ...33
B. Taarifa ya Malazi Nchini Ufaransa................36
C. Ratiba ya Kongamano...............................37
D. Baadhi ya Ikisiri za Kongamano....................41

Nukuu Baba wa Taifa, Mwl. Julius K Nyerere,
Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania....48



# Ujumbe wa Waziri

Kwa heshima na taadhima, ninapenda kuwakaribisha washiriki wote wa Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa, litakalofanyika Makao Makuu ya UNESCO, Paris, Ufaransa, kuanzia tarehe 4 hadi 7 Julai 2026. Hili ni tukio la kihistoria linaloendelea kuthibitisha nafasi ya Tanzania na Bara la Afrika katika kukuza na kueneza lugha adhimu na aushi ya Kiswahili duniani.

Kongamano hili limepata heshima ya kufanyika sambamba na Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yanayofanyika kila tarehe 7 Julai, hatua inayosisitiza dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Jemedari Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutumia Kiswahili kama chombo cha kuimarisha uhusiano wa kimataifa, kuendeleza amani, na kuhimiza diplomasia ya kiuchumi. Kupitia kongamano hili, tunakusudia kuonesha kuwa Kiswahili ni zaidi ya chombo cha mawasiliano, ni urithi wa kiutamaduni, nyenzo ya maendeleo, na daraja la kuunganisha mataifa.

Kaulimbiu ya Kongamano hili, "Kiswahili kwa Amani, Mshikamano na Diplomasia ya Uchumi Duniani" inaakisi dhamira ya kutumia Kiswahili kama chachu ya kujenga ushirikiano wa kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa. Kongamano hili ni fursa ya kuimarisha nafasi ya Kiswahili kama lugha ya kidiplomasia inayoweza kushiriki kikamilifu katika ajenda za kimataifa za amani, maendeleo, na ustawi wa jamii.

Ninakushukuruni nyote mliofanikisha maandalizi ya kongamano hili, hususan UNESCO, Serikali ya Ufaransa, wizara za kisekta, mabaraza ya Kiswahili, vyama vya Kiswahili, wawasilishaji wa makala, wajasiriamali, na wanahabari. Ushirikiano wenu ni muhimu katika kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kujenga utangamano wa kimataifa.

Tanzania itaendelea kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inaendelezwa kwa kasi inayotakiwa. Ninawatakia washiriki wote Kongamano lenye tija na matokeo chanya kwa maendeleo ya Kiswahili kitaifa, kikanda na kimataifa.

**Asante sana.**

**Paul Christian Makonda (Mb.),**
**Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo,**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**



# Dibaji

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa ambalo ni jukwaa muhimu la kustawisha matumizi ya Kiswahili duniani. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka nia ya dhati ya kuhakikisha Kiswahili kinaweka mizizi yake barani Ulaya.

Kongamano hili ambalo litaambatana na Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili litahudhuriwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ndiye Mgeni Rasmi. Ushiriki wa Mhe. Rais katika tukio hili ni ishara ya heshima kubwa ambayo Serikali inaipa lugha ya Kiswahili kama urithi wa taifa, utambulisho wa Waafrika na daraja la ushirikiano wa kimataifa. Aidha, huu ni uthibitisho wa mchango mkubwa wa Tanzania katika kukuza na kueneza Kiswahili duniani.

Maandalizi ya kongamano hili yamezingatia umuhimu wa kuwapatia washiriki taarifa sahihi na mwongozo thabiti utakaowasaidia katika safari na ushiriki wao kwa ujumla. Hivyo, Mwongozo huu umeandaliwa mahsusi ili kutoa maelekezo muhimu kuhusu maandalizi ya safari, taratibu za usafiri, maisha nchini Ufaransa, pamoja na ratiba na shughuli mbalimbali zitakazofanyika wakati wa kongamano.

Ninawasihi washiriki wote kuusoma na kuutumia ipasavyo ili kujipanga vizuri katika kuliwakilisha vyema taifa, lugha na utamaduni wetu kwa ujumla. Aidha, ni matarajio yangu kuwa Kongamano hili litazidi kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika kukuza na kueneza Kiswahili na kufungua fursa mpya za kidiplomasia, kiuchumi, na kiutamaduni.

Kwa niaba ya Serikali, ninawapongeza washirika wote, na kwa namna ya pekee UNESCO, kwa kufanikisha kongamano hili. Pia, ninawatakia washiriki wote safari njema, ushiriki wenye mafanikio na kumbukumbu nzuri wakati wote wa Kongamano nchini Ufaransa.

**Gerson P. Msigwa**
**Katibu Mkuu - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo & Msemaji Mkuu wa Serikali**



# Salamu za Ukaribisho

Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa na Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania UNESCO unayo furaha kuwakaribisha washiriki wote wa Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa hapa jijini Paris, Ufaransa tarehe 4-7 Julai 2026. Mgeni Rasmi wa Kongamano hili atakuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ubalozi wa Tanzania nchini Ufaransa unayo heshima kuwa mwenyeji wa Kongamano hili. Hivyo, utaendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi zote zinazohusika ili kuhakikisha wageni na washiriki wote wa Kongamano wanapata huduma na ushirikiano unaostahili katika kipindi chote cha kongamano.

Kwa niaba ya Ubalozi na Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania UNESCO, ninakukaribisheni nyote jijini Paris na ninakutakieni ushiriki wenye mafanikio na fanaka muwapo nchini Ufaransa.

**KARIBUNI SANA!**

**Saidi Othman Yakubu, FCG,**
**Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa, & Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania UNESCO.**

# SEHEMU YA KWANZA
# UTANGULIZI WA JUMLA



## Usuli wa Kongamano

Kiswahili kimeendelea kukua, kuenea, kutambuliwa, na kutumika kila upande duniani. Aidha, Kiswahili ni miongoni mwa lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika, na Umoja wa Wazalishaji Almasi Afrika. Kwa upande wa Umoja wa Mataifa, UNESCO imetangaza tarehe 7 Julai kila mwaka kuwa ni Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani na kuridhia Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha rasmi katika Mkutano Mkuu wa UNESCO.

Kwa kuzingatia usuli huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo, imeshirikiana na UNESCO kuandaa Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa. Kongamano hili litafanyika tarehe 4-7 Julai 2026 jijini Paris, Ufaransa, katika viunga vya makao makuu ya UNESCO, sambamba na Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU). Kaulimbiu ya Kongamano hili ni "Kiswahili kwa Amani, Mshikamano, na Diplomasia ya Uchumi Duniani".

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imebeba sehemu kubwa ya gharama za maandalizi ya Kongamano. Kwa upande wake, UNESCO imechangia kutoa kumbi za kufanyia Kongamano, eneo la kufanyia maonesho, vifaa mbalimbali vya kufanikisha Kongamano (kama vile vifaa vya ukalimani), msaada wa kitaalamu, pamoja na kujenga daraja baina ya taasisi za Tanzania na asasi mbalimbali za kimataifa ili kuanzisha ushirikiano.

Hatua mbalimbali za maandalizi ya Kongamano hili zimehusisha wizara za kisekta, zikiwamo: Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mgeni Rasmi katika Kongamano hili ni **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**




## Malengo ya Kongamano

Kongamano hili lina malengo ya aina mbili, lengo kuu na malengo mahususi.

## Lengo Kuu

Kukuza na kueneza Kiswahili katika ukanda wa Ulaya na kukitumia kama mojawapo ya nyenzo za kuimarisha maslahi mapana ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, na kidiplomasia.

## Malengo Mahsusi

a. Kukikuza na kukieneza Kiswahili katika nchi za Ulaya; na
b. Kuimarisha uhusiano wa kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi za Ulaya kwa ujumla.



## Matokeo ya Kongamano la Kwanza

Kufanyika kwa Kongamano la Pili kunachagizwa na matokeo ya Kongamano la Kwanza la Kiswahili la Kimataifa lililofanyika tarehe 7 - 10 Novemba 2024, jijini Havana, Matokeo hayo ni:

a. Kufunguliwa kwa vituo viwili vya kufundisha Kiswahili katika Ukanda wa Karibe na Marekani;
b. Kiswahili kimeendelea kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Havana;
c. Baadhi ya mikataba ya ushirikiano imezaa matunda. Mathalani, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kimeanza kufundisha lugha ya Kihispaniola kwa kutumia walimu wawili kutoka Chuo Kikuu cha Havana;
d. Kuhusishwa kwa mara ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili katika maadhimisho ya utamaduni nchini Kuba; na
e. Kupatikana kwa machapisho ya kufundishia Kiswahili nchini Kuba.

Kongamano hili litahusisha washiriki walio katika makundi mbalimbali, yakiwamo: wakuu wa nchi, viongozi wa asasi za kimataifa, mawaziri, mabalozi, makatibu wakuu wa wizara, wadau wa sekta binafsi, wadau wa idhaa zinazotangaza kwa lugha ya Kiswahili, wadau wa vyama vya Kiswahili, wadau wa taasisi na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali (ya kitaifa na ya kimataifa), wajasiriamali, na wasanii. Ufuatao ni mchanganuo wa makundi haya.

a. **Wakuu wa nchi:** Mbali na mgeni rasmi ambaye ni Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wamealikwa pia marais wa nchi mbalimbali, wakiwamo: Mhe. Azali Assoumani, Rais wa Jamhuri ya Umoja wa Visiwa vya Comoro, na Mhe. Evariste Ndayishimeye, Rais Jamhuri ya Burundi,

b. **Viongozi wa asasi za kimataifa:** Kongamano hili litahudhuriwa na Mhe. Prof. Khaled Eli-Enany Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO (DG UNESCO). Aidha, Kongamano linatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi wa asasi nyingine za kimataifa, kama vile ILO, WHO, UNDP, FAO, UNICEF, WFP, UNHCR, UN-Women, IMF, na UN-Habitat.

c. **Mawaziri:** Mawaziri mbalimbali wanatarajiwa kushiriki katika Kongamano hili. Miongoni mwao ni: Mhe. Paul Christian Makonda (Mb) Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Riziki Pembe Juma (Mb), Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, na Mhe. Mahamudu Thabit Kombo (Mb) Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

d. **Mabalozi:** Mbali na Mhe. Said Yakub FCG, Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa, Mwakilishi wa kudumu wa UNESCO, ambaye ni mwenyeji wa Kongamano, pia kutakuwa na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali, na mabalozi mbalimbali wanaoziwakilisha nchi zao nchini Ufaransa.

e. **Makatibu wakuu wa wizara:** Makatibu mbalimbali wanatarajiwa kushiriki katika Kongamano hili. Miongoni mwao ni Bw. Gerson P. Msigwa—Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Bw. Mattar Zahor Masoud—Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

f. **Wadau wa sekta binafsi:** Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo ya taifa kupitia lugha ya Kiswahili, Kongamano hili linatarajiwa kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta binafsi.

g. **Wadau wa idhaa zinazotangaza kwa lugha ya Kiswahili:** Kongamano litahudhuriwa na waandishi wa habari na watangazaji wa redio na televisheni zinazotoa huduma kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Mifano ya idhaa hizo ni: Radio France International (RFI), Deutch Welle (DW), British Broadcasting Corporation (BBC), Russia Today (RT), na Sauti ya Amerika.

h. **Wadau wa vyama vya Kiswahili:** Wanachama na wapenzi wa vyama vya Kiswahili vya kitaifa, kikanda, na kimataifa, watashiriki Kongamano hili. Miongoni mwa vyama hivyo ni: Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), Chama cha Wahadhiri wa Kiswahili Afrika


Mashariki (CHAKAMA), na Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU). Kundi hili la washiriki linajumuisha wahadhiri, walimu, na wanafunzi wa Kiswahili. Pamoja na mambo mengine, wadau hawa watashikiri kuwasilisha makala mbalimbali za kitaaluma.

j. **Wadau wa taasisi na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali (ya kitaifa na ya kimataifa):** Washiriki wa kundi hili wamealikwa ili kukidhi kiini cha kaulimbiu ya Kongamano hili—"Kiswahili kwa Amani, Mshikamano, na Diplomasia ya Uchumi Duniani". Washiriki wa kundi hili watachochea kuanzishwa au/na kuimarishwa kwa utangamano wa kijamii, kiuchumi, na kidiplomasia kupitia lugha na utamaduni wa Kiswahili baina ya Watanzania na jamii nyinginezo.

k. **Wajasiriamali:** Kongamano litahudhuriwa na wajasiriamali wa nyuga mbalimbali zinazohusiana na lugha na utamaduni wa Mswahili. Wajasiriamali hao watanufaika kwa kuonesha huduma na/au bidhaa zao. Pia, kupitia vikao au mazungumzo na wadau wa kutoka katika jamii nyingine, wataweza kupata fursa ya kuanzisha na/au kuimarisha ushirikiano wa kibiashara.

l. **Wasanii:** Wadau wa sanaa za aina mbalimbali watashiriki Kongamano hili. Mifano ya sanaa hizo ni ushairi, ngoma za jadi, sarakasi, na muziki (kama vile taarabu, bongo fleva, singeli).

## Washiriki Jumla: 1000




| | | |
|---|---|---|
| Watanzania | 500 | (50%) |
| Diaspora | 200 | (20%) |
| Wageni toka Mataifa ya Afrika | 150 | (15%) |
| Wageni toka Mataifa ya Ulaya, Amerika Kaskazini, Amerika Kusini, Asia, India na China | 150 | (15%) |

**Jumla: 1000 (100%)**

# SEHEMU YA PILI:
# MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA

## Usajili

Washiriki wa Kongamano hili wanapaswa kuwa wamejisajili kupitia kiungo kifuatacho: *http://edodoso.gov.go.tz/index.php?r=survey/index&sid=725913&newtest=Y&lang=en*

## Mahitaji ya Viza

Washiriki wa Kongamano watatakiwa kuomba viza. Maombi ya viza yatafanywa kwa kufuata hatua mbili.

1. Hatua ya kwanza inayohusu ujazaji wa fomu ya maombi itatakiwa kutekelezwa kupitia kiungo kifuatacho: *https://france-visas.gouv.fr/en/online-application*.
2. Hatua ya pili inayohusu uwekaji wa miadi itatakiwa kutekelezwa kupitia kiungo kifuatacho: *https://visas-fr.tlscontact.com*.

Washiriki wa wenye hati za kusafiria zenye hadhi ya kidiplomasia (diplomatic passport) na huduma (service passport) watahudumiwa kulingana na hadhi ya hati hizo.

## Bima ya Safari

Kila mshiriki anapaswa kuwa na bima ya safari. Bima hiyo inaweza kupatikana kupitia kiungo kifuatacho: https://wa.me/255764166066?text=bimapap au kwa kubofya ***150*51#** katika simu. Ikiwa mshiriki atahitaji msaada, anaweza kupiga namba **+255711424205**.

## Chanjo na Huduma za Afya

Washiriki wote wanapaswa kuwa na kadi ya chanjo ya homa ya manjano ili kuingia katika nchi ya Ufaransa. Mshiriki asiye na kadi hii anaweza kufanya mchakato wa kuipata kupitia: https://afyamsafiri.moh.go.tz/. Pia, washiriki wanaotumia dawa/dozi za muda mrefu wanashauriwa kwenda na dawa zao. Zaidi ya hayo, washiriki wanasisitizwa kubeba dawa kama vile panadol na flagyl.

## Upatikanaji wa Mahitaji Muhimu

a. Washiriki wote wanashauriwa kununua kabisa mahitaji muhimu ya kila siku kama vile miswaki, dawa za meno, na mafuta ili kupunguza gharama. Hii ni kwa sababu maisha ya jijini Paris ni ghali sana.

b. Washiriki wanapaswa kuandaa nyenzo za kuchajia vifaa vya umeme (kama vile simu, vishikwambi, na kompyuta) zinazoendana na mifumo ya umeme ya nchi za Ulaya. Mifumo hiyo hutumia matundu mawili (badala ya matatu ambayo hutumika katika nchi nyingi za Afrika, ikiwamo Tanzania).

## Gharama za Usafiri na Malazi

Washiriki wote watajitegemea kwa usafiri na malazi. Kila mshiriki atatakiwa kuwekesha kwa ajili ya huduma hizo (ndege na hoteli) kwa gharama zake binafsi.

## Gharama za Mashirika Mbalimbali ya Ndege

Makadirio ya gharama za tiketi kwa mashirika mbalimbali ya ndege kwa kipindi hiki cha mwezi Mei 2026 zimeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Shirika | Nauli kwa Daraja la Uchumi (SHT) | Nauli kwa Daraja la Biashara (SHT) | Vituo vya Kutua & Muda wa Kusafiri |
|---|---|---|---|
| Emirates | 3,031,000 | 15,070,000 | Dubai – Saa 4 na dk 20 |
| Qatar Airways | 2,857,000 | 10,241,000 | Doha – Saa 3 na dk 45 |
| Turkish Airlines | 4,105,530 | 8,224,000 | Istanbul – Saa 6 na dk 40 |
| Kenya Airways | 4,656,000 | 13,961,000 | Nairobi – Paris, Saa 2 na dk 30 |
| Ethiopian Airlines | 5,904,720 | 10,513,000 | Addis Ababa – Paris, Saa 2 na dk 30 |
| KLM | 6,201,360 | 16,545,000 | Amsterdam – Paris, Saa 2 na dk 30 |
| Air France | 9,596,000 | 21,313,000 | Nairobi – Paris, Saa 2 na dk 30 |




## Utaratibu wa Safari ya Kwenda kwenye Kongamano

Ili kurahisisha safari kwa washiriki, sekretarieti inaandaa utaratibu wa kusafiri kwa pamoja. Washiriki watasafiri kuelekea Paris kwa makundi matatu. Kundi la kwanza litasafiri Juni 20, 2026. Kundi hili litahusisha wajumbe wachache wa sekretarieti ya maandalizi. Kundi la pili litasafiri Juni 30, 2026. Kundi hili litahusisha viongozi mbalimbali wa Wizara za kisekta. Kundi la tatu litasafiri Julai 2, 2026. Kundi hili litahusisha washiriki wengine wote, wakiwamo wawasilishaji wa mada na wasanii. Safari ya kurudi kwa makundi yote itakuwa Julai 8, 2026.

# Utaratibu wa Mavazi Wakati wa Kongamano

Washiriki wa Kongamano watazingatia utaratibu wa mavazi ambao umeelezwa katika jedwali lifuatalo:

| Tarehe | Tukio | Utaratibu wa Mavazi |
|---|---|---|
| Julai 4, 2026 | Ufunguzi, maandamano, na ziara | Vazi la Kimaasai & kanga 4 kati ya zinazopendekezwa kati mchakato wa kusaka vazi la taifa |
| Julai 5, 2026 | Tamasha la Kiswahili & Usiku wa Mswahili | Vazi la kitamaduni (kv. Kanzu, mabaibui, baraghashia, kanga—zikiwamo zinazopendekezwa katika mchakato wa kusaka vazi la taifa) |
| Julai 6, 2026 | Uwasilishaji wa makala | Vazi rasmi la kiofisi |
| Julai 7, 2026 | Kilele cha MASIKIDU | Vazi rasmi la kiofisi |



## Hali ya Hewa

Hali ya hewa ya nchini Ufaransa kwa mwezi wa saba huwa ya baridi kiasi, ikiwa na wastani wa nyuzi 25-26 wakati wa mchana na nyuzi 15-16 wakati wa jioni na usiku. Hivyo, washiriki wanashauriwa kujiandaa kwa mavazi yanayoendana na kuikabili hali hii.

## Mkakati wa Mawasiliano

Umeandaliwa mkakati wa kuelimisha umma kuhusu Kongamano. Mkakati huo unaolenga kutoa taarifa za kabla, wakati na baada ya Kongamano unahusisha hatua zifuatazo:

a. Kuandaa vipeperushi vya kunadi Kongamano. Vipeperushi hivyo vitarushwa katika mitandao ya kijamii yenye wafuasi wengi na mitandao ya wizara za kisekta na taasisi zake.

b. Kuandaa matangazo mafupi ya picha jongevu yatakayotumika kwenye treni za kisasa, vituo vya televisheni (kama vile TBC, Channel Ten, Azam, na ITV), mfumo wa mawasiliano ya Serikali na kwenye mitandao ya kijamii.

c. Kushirikisha watu maarufu mwenye wafuasi wengi katika matangazo.

d. Kuandaa mkutano wa wanahabari na Waziri wa HUSM kuelezea maandalizi ya kongamano.

e. Wajumbe wa sekretarieti kushiriki vipindi vya redio na televisheni, hususan vinavyohusiana na Kiswahili, kwa ajili ya kulitangaza Kongamano na kufanya tathmini baada ya Kongamano.

f. Viongozi wa Wizara ya HUSM na wahusika wa Ubalozi wa Tanzania nchini Ufaransa kushiriki katika kulitangaza Kongamano kupitia vyombo vya habari vinavyorusha matangazo yake nchini Ufaransa.

g. Kurusha matangazo mubashara ya matukio yote kuanzia Julai 4 - 7, 2026.

h. Baada ya Kongamano, kuandaa makala na jarida maalum kuhusiana na tukio zima

## Njia za Mawasiliano Nchini Ufaransa

Mitandao mbalimbali ya simu inayopatikana nchini Tanzania inaweza kufanya kazi pia nchini Ufaransa. Aidha, mitandao ya kijamii kama vile facebook, Instagram, WhatsApp, Imo, X, na Threads inafanya kazi nchini Ufaransa.

## Mawasiliano kuhusu Kongamano

Anwani za mawasiliano UNESCO ni:

UNESCO HQ
7 Place de Fontenoy
75007 Paris.



## Watu wa kuwasiliana nao ni:

a. Bi. Sekela Mwambegele:

- Simu: +33601959731 (kwa WhatsApp tu)
- Baruapepe: sekela.mwambegele@nje.go.tz

b. Bw. Aggrey Meena:

- Simu: +33678519040 (kwa WhatsApp tu)
- Baruapepe: aggrey.meena@nje.go.tz

c. Bi. Eva Mashala:

- Simu: +33611143849 (kwa WhatsApp tu)
- Baruapepe: eva.mashala@nje.go.tz

# SEHEMU YA TATU:
# MATUKIO YA KONGAMANO



## Ufunguzi wa Kongamano

Kongamano litafunguliwa tarehe 4 Julai 2026 saa nane mchana katika viunga vya makao makuu ya UNESCO.

## Ziara

Julai 4, 2026 kuanzia saa nane mchana washiriki watapata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali, kama vile Mnara wa Eiffel na Mto Seine.

## Uwasilishaji wa Makala za Kitaaluma

Makala thelathini na mbili (32) zinazoongozwa na kaulimbiu ya Kongamano "Kiswahili kwa Amani, Mshikamano, na Diplomasia ya Uchumi Duniani" zinatarajiwa kuwasilishwa tarehe 6 Julai 2026 kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Makala hizo zitawasilishwa katika majopo yatakayokuwa katika vyumba vitatu. Kila makala itatengewa wastani wa dakika 20 za uwasilishaji na mjadala wake. Jedwali lifuatalo linaonesha washiriki wanaotarajiwa kuwasilisha makala hizo:

| # | Mada ya Makala | Jina la Mwasilishaji na Nchi Anayotoka |
|---|---|---|
| 1. | Tafsiri kama Diplomasia ya Kitamaduni: Abdulrazak Gurnah na Utambulisho wa Kiswahili | Ida Hadjivayanis - Uingereza |
| 2. | Kiswahili na Vijana | Zawadi Sakapalla - Tanzania |
| 3. | Mchango wa Riwaya ya Kiswahili katika Kufundisha Diplomasia: Mfano wa Riwaya ya *Kusadikika* | Athumani S. Ponera - Tanzania |
| 4. | Ukiona Vyaelea Vimeundwa: Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani | Mussa. M. Hans - Tanzania |
| 5. | Ufanisi wa Kiswahili katika Kujenga Umoja na Maendeleo Madhubuti ya Afrika Kupitia Teknolojia ya Akili Unde (AU) | Aldin Mutembei - Tanzania |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Mdhihiriko wa Mitindo ya Lugha katika Hotuba za Rais Dkt. Mwinyi katika Kuhimiza Amani, Mshikamano na Maendeleo | Riziki Pembe Juma & Ahmad Y. Sovu-Tanzania |
| 7. | Kiswahili na Uchumi | Ibrahima Ibrahim - Comoro |
| 8. | Ubunifu wa Kaulimbiu za Kiswahili za Kuhamasisha Amani Nchini Tanzania | Alpha Kavishe, Issaya Lupogo & Mustapha Almasi - Tanzania |
| 9. | Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza Uchumi wa Taifa la Tanzania | Anna N. Kyamba - Tanzania |
| 10. | Utani kama Nyenzo ya kukuza Uchumi wa Biashara: Mifano kutoka kwenye Masoko ya Jadi | Asifiwe Mwagike - Tanzania |
| 11. | Kusimamia Haki ya Kijamii Darasani: Uchunguzi wa Mbinu za Ukuzaji wa Kiswahili katika Mazingira ya Kielimu Yenye Lugha Nyingi | Said S. Khassim - Uholanzi |
| 12. | Sera ya lugha nchini Burundi na athari zake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili | Bamporubusa Mathieu - Burundi |
| 13. | Nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika Kujenga na Kudumisha Amani Afrika Mashariki | Benitha France - Tanzania |
| 14. | Kiswahili na Diplomasia | Chifu Said Mohamed Said (Chifu Kapere) - Tanzania |

| | | |
|---|---|---|
| 15. | Nafasi ya Muziki katika Kujenga Utangamano wa Kimataifa | Adria Fuluge & Davian Buguna - Tanzania |
| 16. | Matumizi ya Akiliunde kama Nyenzo ya Tafsiri katika Ujifunzaji wa Kiswahili: Uzoefu Kutoka Chuo Kikuu cha Ghana | Hadija Jilala - Tanzania |
| 17. | Nguvu ya Kiswahili Katika Diplomasia ya Kitamaduni na Maendeleo ya Utalii | Lorna B. Mwijarubi - Tanzania |
| 18. | Dhima ya Kisw ahili katika ElimuMsingi: Chimbuko la Wana Diplomasia Bobevu | Maryam Y. Mwinyi - Tanzania |
| 19. | Mapitio ya Nafasi ya Kiswahili katika Utangamano wa Kimataifa kwa jicho la Ubuntu | Meinrad Haule Lembuka - Tanzania |
| 20. | Tafsiri katika Kiswahili na Mabadiliko ya Uchumi wa Kidijiti | Amour S. Said Zanzibar - Tanzania |
| 21. | Nafasi ya Akiliunde kati ka Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Mkabala wa Kimawasiliano | Nasra Habibu na Salma Hamad - Tanzania |
| 22. | Kiswahili: Msingi wa Uhuru wa Kidijitali kwa Vijana | Onesmo S. Nyinondi - Tanzania |
| 23. | Dhima ya Kiswahili katika Kujenga Utambulisho wa Kitaifa Kupitia Mfumo wa Elimu | Saade Said Mbarouk na Mwanahija Ali Juma - Tanzania |
| 24. | Mchango wa Akiliunde katika Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kwenye Diplomasia ya Kidijit i na Uchumi wa Dunia | Shaban Rashid Said - Tanzania |

| | | |
|---|---|---|
| 25. | Onomastiki ya Ulem avu katika Methali za Waswahili: Elimu kwa Mtzamo wa Maarifa Asili | Wanjala Simiyu - Kenya |
| 26. | Urazini wa Diplomasia ya Uchumi katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Makuwadi wa Soko Huria* (Chachage, 2002) | Stela Faustine-Tanzania |
| 27. | Maendeleo ya Elimu ya Kiswahili Duniani: Mifano kutoka nchini China na Marekani | Caesar Jjingo - Uganda |
| 28. | Uchanganuzi wa Kimaeneo wa Matumizi ya Kiswahili katika Huduma za Utalii kwa Wageni Nchini Tanzania | Theresia Bonface Mbogo - Tanzania |
| 29. | Nafasi ya Kiswahili katika kujenga utangamano wa kimataifa nchini Uganda | Monday Geofrey Akol Amazima - Uganda |
| 30. | Mbinu za Uhunthishaji wa Wahusika katika Filamu za Kiswahili: Mifano kutoka Vichekesho vya Joti na Dulvani. | Diana Remias - Tanzania |
| 31.. | Kiswahili na Amani | Elizabeth Luena Lyimma - Tanzania |
| 32. | Kiswahili katika Ustawi wa Vijana na Nafasi Yake katika Kudumisha Amani na Maendeleo Endelevu kwa Vijana Afrika Mashariki | Ali Haji Hassan - Tanzania |









## Tamasha la Kiswahili

Kutakuwa na tamasha litakalofanyika katika viunga vya Mnara wa Eiffel. Miongoni mwa matukio yatakayojiri katika tamasha hilo ni hafla ya Usiku wa Mswahili ambao utahusisha maonesho mbalimbali ya kiutamaduni na burudani. Pia, tamasha litapambwa na mavazi yanayoonesha utambulisho wa Mswahili.







## Maonesho Mbalimbali

Kutakuwa na maonesho fursa na nafasi ya Kiswahili kama kibebeo katika nyanja mbalimbali. Maonesho yatakayoshirikiswa katika kongamano hili ni pamoja na:

a. **Maonesho ya Kilimo:** Sampuli za kahawa, chai, korosho, katani, pamba, viungo na mazao ya bustani kutoka Tanzania. Pia, Video au picha zinazoonesha safari ya zao kutoka shambani hadi sokoni. Maonesho ya teknolojia za kisasa za kilimo Tanzania. Ujumbe wa Kiswahili kama "Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi."

b. **Maonesho ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu:** Bidhaa za samaki, mwani, na bidhaa za baharini. Picha za ziwa Victoria, bahari ya Hindi na maeneo ya uvuvi Tanzania. Maelezo kuhusu uchumi wa buluu kwa Kiswahili na lugha ya wenyeji

c. **Maonesho ya Madini:** Sampuli au replicas za madini kama Tanzanite, dhahabu, almasi zitaoneshwa. Ramani ya maeneo ya madini na aina ya madini Tanzania. Historia ya mchango wa sekta ya madini katika maendeleo.

d. **Maonesho ya Viwanda na Uzalishaji wa Tanzania:** Bidhaa zilizotengenezwa Tanzania: nguo, sabuni, ngozi, vyakula vilivyosindikwa zitoneshwa. Maonesho ya miradi kama Standard Gauge Railway kama ishara ya ukuaji wa viwanda. Zana zote ziwe na Ujumbe: "Made in Tanzania."

e. **Maonesho ya Utalii na Urithi wa Taifa:** Picha, video au ramani za Mlima Kilimanjaro, Hifadhi taifa ya Serengeti, Mji mkongwe. Muziki, mavazi, vyakula na sanaa za asili.

**Maonesho ya Sanaa, Muziki na Filamu:** Muziki wa Bongo Flava, ngoma za asili, mashairi na tamthilia. Uchoraji wa Tingatinga, vinyago, kazi za mikono. Ujumbe wa Kiswahili kupitia sanaa na ubunifu.

f. **Maonesho ya Siasa, Diplomasia na Uongozi:** Maonesho ya Historia ya uhuru, Muungano, na diplomasia ya Tanzania. Pia kutaoneshwa maonesho ya Historia ya Ukombozi wa Afrika. Nukuu za viongozi kama Julius Nyerere na Samia Suluhu Hassan zitachezwa kwenye screen kubwa. Pia maonesho ya mchango wa Kiswahili katika diplomasia ya Afrika.

g. **Maonesho ya Teknolojia na Ubunifu:** Apps, mifumo ya kidijitali, fintech na elimu mtandao. Kampuni za ubunifu kutoka Tanzania. Ujumbe: "Kiswahili kwa Amani, Mshikamano na Diplomasia ya Uchumi."

h. **Maonesho ya vitabu vya Lugha ya Kiswahili na Kifaransa:** Vitabu vya Swahili, kamusi, tafsiri, mashairi, methali na misemo.




## Burudani

Kongamano hili litanogeshwa na burudani mbalimbali, zikiwamo:

a. **Muziki wa Asili:** Muziki huu unalenga kuonesha tamaduni za makabila mbalimbali kupitia nyimbo, ngoma na ala za jadi. Mifano ya vikundi vinavyotarajiwa kuwapo ni Magoma Moto na Safi theatre.

b. **Taarab:** Hii ni burudani ya muziki wa Kiswahili wenye mashairi na ala za kitamaduni. Katika kundi hili, tunatarajia kupata burudani kutoka kwa wanamuziki mahiri na vikundi vya taarab vya Tanzania.

c. **Ngonjera na Ushairi:** Kwa kawaida, waimbaji katika kundi hili huigiza, huimba na kughani mashairi ya Kiswahili. Burudani hii itawashirikisha wanafunzi na vikundi vya washairi wa vyuo vikuu.

d. **Muziki wa Kisasa wa Kiswahili:** Kongamano litapambwa na burudani ya muziki wa kizazi kipya unaotumia Kiswahili. Mifano ya wasanii wa kundi hili ni Diamond Platnumz na Harmonize.

e. **Sanaa ya Maigizo:** Burudani hii itahusisha tamthilia zenye ujumbe wa lugha, utamaduni na maadili. Mifano ya vikundi hivyo ni: vikundi vya sanaa vya vyuo vikuu na vikundi vya maigizo vya jamii.

f. **Sarakasi na akrobatiki:** Hili litaonesha vipaji vya mwili, michezo ya jukwaani na vichekesho. Mifano ya vikundi hivyo ni: Vikundi vya sarakasi vya vijana na makundi ya acrobatics ya mitaani toka Tanzania na mataifa mbalimbali.

## Vikao vya Miadi na Tete-a-tete

Kongamano hili litatoa fursa kwa wadau mbalimbali kufanya mazungumzo yanayolenga kuimarisha uhusiano wa kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, na kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi mbalimbali, hususan za Ulaya.






## Uzinduzi wa Machapisho

Machapisho mbalimbali yanayohusiana na lugha na utamaduni wa Kiswahili yanatarajiwa kuzinduliwa. Baadhi yayo ni:

a. Kitabu cha misemo kiitwacho “Kiswahili-Kiingereza-Kihausa”,
b. Kitabu cha misemo ya kila siku kiitwacho “Kiswahili-Kiingereza-Kifaransa”, na
c. Kamusi ya Kifaransa-Kiswahili.



# Utiaji Saini wa Hati za Makubaliano na Ushirikiano

Hati mbalimbali za makubaliano na ushirikiano zinatarajiwa kujadiliwa au/na kusainiwa kwa lengo la kuendeleza ushirikiano baina ya sekta mbalimbali zilizopo nchi Tanzania na zile zinazopatikana nchini Ufaransa. Miongoni mwa hati zinazotarajiwa kusainiwa zitahusisha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Taasisi ya Elimu Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania. Mikataba hiyo pia itahusisha Asasi zenye majukumu yanayofanana na masuala hayo nchini Ufaransa.



## Utoaji wa Tuzo

Katika kongamano hili, zitatolewa tuzo kwa mashirika, taasisi, pamoja na watu binafsi kwa lengo la kutambua mchango wao katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

## Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani

Tukio hili litafanyika tarehe 7 Julai 2026 katika viunga vya makao makuu ya UNESCO kuanzia saa nane mchana. Litajumuisha salamu kutoka kwa viongozi mbalimbali na kuhitimishwa na hotuba itakayotolewa na mgeni rasmi, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

# SEHEMU YA NNE: HITIMISHO



## Wito kwa Washiriki

Ni matarajio ya Wizara ya Hahari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo kuwa washiriki watanufaika na mwongozo huu, hivyo kurahisisha maandalizi na ushiriki wao katika Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa. Ni vema washiriki wausome kwa umakini na kujiandaa kikamilifu ili kufikia kilele cha ufanisi wa malengo ya Kongamano.







# 2027 Tanzania Haitapoa: Karibuni kwa Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika (AFCON) na Mlimbwende wa Dunia (Miss World)

Baada ya kumalizika kwa Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa nchini Ufaransa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itazama katika kukamilisha maandalizi ya matukio makubwa mawili yatakayofanyika mwaka 2027 ndani ya nchi yetu. Tukio la kwanza ni Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Mataifa ya Afrika, maarufu kama AFCON. Tanzania itashirikiana na nchi za Kenya na Uganda kuwa wenyeji wa mashindano hayo kuanzia mwezi Januari hadi Februari 2027. Tukio la pili ni Mashindano ya Mlimbwende wa Dunia, maarufu kama Miss World. Kwa mwaka 2027, Tanzania itakuwa mwenyeji wa mashindano hayo yatakayofanyika mwezi Mei.

Kama ilivyo kwa tukio la Kongamano la Paris, kinara wa maandalizi na uratibu wa matukio hayo yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027 pia ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo ambayo itashirikiana na wizara nyingine za kisekta. Kwa kuzingatia kuwa matukio yote mawili—AFCON na Miss World—yatahusisha idadi kubwa ya wageni kutoka kona mbalimbali za Bara la Afrika na duniani mtawalia, ni wazi kuwa zitakuwa fursa nyingine muhimu za kuzidi kuifungua Tanzania kiuchumi, kidiplomasia, na kiutamaduni. Hivyo, ni vema wadau wote tukaendelea kushikamana ili kuyafanikisha matukio hayo mawili.

# VIAMBATISHO:




## A. Mwongozo wa Kupata Viza

Washiriki wa Kongamano wanatakiwa kufanya maombi ya viza kwa njia ya mtandao kwa kufuata hatua zifuatazo:

Kila mshiriki atatakiwa kuomba viza yake binafsi kwa njia ya mtandao (online) kwa kujaza fomu ya maombi kupitia mfumo rasmi wa viza wa Ufaransa kwa kutumia kiungo *https://france-visas.gouv.fr/en/online-application*

Baada ya kukamilisha maombi ya viza kwa njia ya mtandao, kila mshiriki ataomba miadi ya kwenda kwa wakala wa viza (TLS Contact) kwa ajili ya kuwasilisha nyaraka na kukamilisha taratibu nyingine zinazohitajika. Miadi hiyo itaombwa kupitia kiungo *https://visas-fr.tlscontact.com*

Baada ya kuweka miadi, utaandaliwa utaratibu wa waombaji kukutana na maafisa wa ubalozi kwa makundi. Waombaji watakaokuwa wamekamilisha kuomba miadi watatangaziwa utaratibu huo. Nyaraka muhimu za kuzingatia/kuwa nazo wakati wa kukutana na maafisa wa ubalozi wa TLS ni:

i. Barua ya mwaliko kutoka Ubalozi wa Tanzania nchini Ufaransa ikiwa na orodha ya washiriki pamoja na namba za pasipoti zao.
ii. Barua ya mwaliko kutoka BAKITA.
iii. Barua ya mwajiri (kwa walioajiriwa).
iv. Taarifa ya benki ya miezi 6 (wasio waajiriwa).
v. Bima ya safari.
vi. Uwekeshaji wa ndege (flight booking).
vii. Uwekeshaji wa chumba cha hoteli (hotel booking).
viii. Ratiba itakayoonesha matukio ya siku zote (travelling internal).
ix. Picha mbili za pasipoti (ambazo mwonekano wake wa nyuma uwe mweupe—white background).
x. Vyeti vya ndoa/watoto (kwa wanaosafiri na wenza wao au/na watoto).
xi. Nakala ya barua kutoka Wizara ya Mambo ya Nje (note verbale)

# Mchanganuo wa Gharama za Viza

**Dar es Salaam (Special circumstances)**

| Kipengele | Kiasi cha makadirio |
|---|---|
| Ada ya viza | Sh. 259,000 |
| Ada ya huduma | Sh. 117,800 |
| Bima ya safari | Sh. 50,000 |
| Nyaraka na picha | Sh. 20,000 |
| Gharama zakuhamisha ofisi na watoa huduma | Sh. 343,601 |
| **Jumla kuu** | **Sh. 790,401** |

**Dodoma na Zanzibar (Special circumstances)**

| Kipengele | Kiasi cha makadirio |
|---|---|
| Ada ya viza | Sh. 259,000 |
| Ada ya huduma | Sh. 117,800 |
| Bima ya safari | Sh. 50,000 |
| Nyaraka na picha | Sh. 20,000 |
| Gharama zakuhamisha ofisi na watoa huduma | Sh. 649,002 |
| **Jumla kuu** | **Sh. 1,095,802** |

## B. Taarifa ya Malazi Nchini Ufaransa

| Jina la Hoteli | Huduma Inayopatikana | Gharama za Mtu Mmoja kwa Chumba kwa siku 6 (Dola za Marekani) | Gharama za Wawu Wawili kwa Chumba kwa siku 6 (Dola za Marekani) | Umbali kutoka Ukumbi wa Kongamano (Km) |
|---|---|---|---|---|
| Waldorf Astoria Versailles - Trianon Palace | Malazi na kifungua kinywa | 2,456.00 | 1,355.00 | 15 |
| Hyatt Place Paris Charles De Gaulle Airport | Malazi na kifungua kinywa | 2,075.00 | 1,195.00 | 35 |
| Aparthotel Adagio Paris Centre Tour Eiffel | Malazi na kifungua kinywa | 1,795.00 | 1165.00 | 2 |
| Nh Paris Gare De L'est | Malazi na kifungua kinywa | 1,665.00 | 990.00 | 7 |
| Mercure Paris 15 Porte De Versailles | Malazi na kifungua kinywa | 1,550.00 | 985.00 | 1.9 |
| Novotel Paris Porte De Versailles | Malazi na kifungua kinywa | 1,450.00 | 980.00 | 3.4 |
| Best Western The Hotel Versailles | Malazi na kifungua kinywa | 1,190.00 | 875.00 | 24.5 |

## C. Ratiba ya Kongamano

**TAREHE 4 JULAI 2026: SIKU YA UFUNGUZI, ZIARA NA KUTEMBELEA WADAU WA KISWAHILI**

| MUDA | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|
| Saa 4:00 asb - 10:50 Jioni | Maandamano ya Kiutamaduni Kuelekea Eiffel Tower na Ziara | Washiriki |
| Saa 4:00 asb - 10:50 Jioni | Ziara katika Taasisi Wadau wa Kiswahili | Washiriki watakaoteuliwa |
| Saa 8:40 - 8:50 Mchana | Viongozi Maalumu Kuwasili Ubalozini | Viongozi Maalumu |
| Saa 8:50 - 9:00 Alasiri | Wimbo wa Taifa la Tanzania | Washiriki |
| Saa 9:00 - 9:10 Alasiri | Burudani | Mshereheshaji |
| Saa 9:10 - 9:25 Alasiri | Utambulisho | Ndugu Gerson Msigwa - Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo |
| Saa 9:25 - 9:35 Alasiri | Salamu za Diaspora | Mwenyekiti wa Diaspora Duniani |
| Saa 9:35 - 9:45 Alasiri | Ukaribisho | Mhe. Balozi Said Yakub |
| Saa 9:45 - 10:20 Jioni | Hotuba ya Mgeni rasmi | Mhe. Paul Christian Makonda - Waziri wa WHUSM |
| Saa 10:20 - 10:30 Jioni | Picha za Pamoja | Mshereheshaji |
| Saa 10:30 - 10:40 Jioni | Viongozi kuondoka Ubalozini | Viongozi Maalumu |

**TAREHE 5 JULAI 2026: SIKU YA MAONESHO**

| MUDA | TUKIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|
| Saa 4:00 - 4:20 Asubuhi | Kuwasili Eiffel Tower | Washiriki |
| Saa 4:20 - 4:30 Asubuhi | Kuwasili kwa Mgeni Maalumu | Mgeni Maalumu |
| Saa 4:30 - 4:40 Asubuhi | Burudani | Kikundi kilichoandaliwa |
| Saa 4:30 - 12:00 Jioni | Maonesho na Burudani | Wote |
| Saa 12:00 - 1:00 Usiku | Maandalizi ya Usiku wa Mswahili | Washiriki |
| Saa 1:00 - 4:00 Usiku | Hafla ya Usiku wa Mswahili<br>• Maonesho ya kiutamaduni<br>• Nasaha za mgeni maalum<br>• Chakula<br>• Burudani<br>ü Bongo fleva<br>ü Singeli<br>ü Taarabu | Wote |
| Saa 4:00 Usiku | Washiriki Kuondoka | Washiriki |

**TAREHE 6 JULAI 2026: MIJADALA YA MADA MBALIMBALI, VIKAO VYA *TETE-A-TETE*, MIADI NA MAONESHO YA UKUMBINI**

| MUDA | TUKIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|
| Saa 3:30 - 3.45 Asubuhi | Kuwasili ukumbini | Washiriki |
| Saa 3:45 - 7:00 Mchana | Uwasilishaji wa Makala - Chumba Na. 200, Chumba Na. 400, na Ukumbi wa Sinema | Wawasilishaji na Washiriki |
| Saa 7:00 - 8:00 Mchana | Chakula cha Asili na Burudani | Washiriki |
| Saa 8:00 - 12:00 Jioni | Uwasilishaji wa Makala - Chumba Na. 200, Chumba Na. 400, na Ukumbi wa Sinema | Wawasilishaji na Washiriki |
| Saa 4:30 - 9:30 Alasiri | Kikao na Mashirika ya Kimataifa<br>Kikao cha Wafanyabiashara na Wawekezaji<br>Kikao cha Usaidizi wa UNESCO katika Kujenga Shule ya Kiswahili | Wafanyabiashara na Wawekezaji |
| Saa 12:00 - 1:00 Usiku | Maonesho ya Makala Jongefu mbalimbali | Washiriki |
| Saa 1:00 - 1:10 Usiku | Kutawanyika | Washiriki |

TAREHE 7JULAI 2026: MAADHIMISHO YA SIKU YA KISWAHILIDUNIANI

| MUDA | TUKIO | WAHUSIKA |
|---|---|---|
| Saa 7:00 - 7:30 Mchana | Kuwasili Makao Makuu ya UNESCO | Washiriki |
| Saa 7:30 - 7:45 Mchana | Kuwasili kwa viongozi | • Mhe. Paul Christian Makonda - Waziri - HUSM<br>• Mhe. Thabit Kombo - Waziri - NJE<br>• Mhe. Azali Assoumani - Rais wa Umoja wa Visiwa vya Comoro<br>• Prof. Khaled EI - Enany Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO |
| Saa 7:45 - 8:00 Mchana | Kuwasili kwa Mgeni Rasmi | Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| Saa 8:00 - 8:10 Mchana | Wimbo wa Taifa la Tanzania | Washiriki |
| Saa 8:10 - 8:30 Mchana | **Utambulisho wa Viongozi na Washiriki** | Ndugu Gerson Msigwa - Katibu Mkuu - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo<br>Mhe. Said Yakubu, Balozi wa Tanzania, Ufaransa |
| Saa 8.40 - 9.10 Alasiri | Salamu za viongozi mbalimbali | • Mwakilishi wa Umoja wa Afrika<br>• Mwakilishi wa Mabalozi wa Ufaransa<br>• Mwakilishi wa vyuo vikuu vinavyofundisha Kiswahili Ufaransa<br>• Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO<br>• Waziri wa HUSM<br>• Waziri wa Mambo ya NJE na UAM<br>• Rais wa Umoja wa Visiwa vya Comoro |

| Saa 9:10 - 9:20 Alasiri | **Burudani** | Kikundi kilichoandaliwa |
|---|---|---|
| Saa 9:20 - 9:35 Alasiri | Uzinduzi wa machapisho | Mgeni Rasmi |
| Saa 9:35 - 9:45 Alasiri | Utiaji Saini | Mgeni Rasmi & Walioandaliwa |
| Saa 9:45 - 10:00 Jioni | Utoaji wa Tuzo | Mgeni Rasmi |
| Saa 10:00 - 11:00 Jioni | Hotuba ya Mgeni Rasmi | Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |
| Saa 11:00 - 11:20 Jioni | Kupiga Picha na Mgeni Rasmi | Mshereheshaji |
| Saa 11:20 - 11:30 Jioni | Burudani | Kikundi kilichoandaliwa |
| Saa 11:30 - 11:40 Jioni | Viongozi Kuondoka Ukumbini | Viongozi |
| Saa 11:40 Jioni | Washiriki Kuondoka Ukumbini | Washiriki |

# Baadhi ya Ikisiri za Kongamano la Pili la Kiswahili la Kimataifa

**Paris, Ufaransa | Julai 4 – 7, 2026**

## Tafsiri kama Diplomasia ya Kitamaduni: Abdulrazak Gurnah na Utambulisho wa Kiswahili

**Ida Hadjivayanis**

ih11@soas.ac.uk

Tafsiri ya fasihi inazidi kuwa chombo muhimu katika diplomasia ya kitamaduni, ikirahisisha usambazaji wa simulizi zinazoendeleza uelewa wa kitamaduni na ule wa uhusiano wa kimataifa. Kwa kutumia tafsiri za kazi za kifasihi za Abdulrazak Gurnah kama kielelezo, wasilisho hili linafafanua jinsi tafsiri inavyofanya kazi ya kuwa kielelezo cha mitazamo ya kidunia na utambulisho wa Waswahili duniani. Kwa kiasi kikubwa, riwaya za Gurnah zilizojikita katika historia binafsi, kumbukumbu za mwambao wa Bahari ya Hindi, na kumbukumbu za ukoloni huchukua maana tofauti zinaposafiri na kuingia katika lugha na tamaduni nyingine. Je, tafsiri hizi huchukua taswira gani zinaporudi katika lugha ya Kiswahili? Tafsiri pekee za Gurnah katika lugha za Kiafrika ni zile zilizofanywa na Hadjivayanis kwa Kiswahili, *Peponi (2022)* na *Dhulma (2025).* Je, tafsiri hizo zina nafasi gani katika diplomasia ya kitamaduni ya Kiswahili? Inakubalika kwamba zinapotafsiriwa katika lugha za kigeni kama Kifaransa na Kichina, hupanua wigo wa wasomaji na kuengua simulizi finyu kuhusu Afrika. Inakuwaje zinaposafiri katika lugha ya Kiswahili?

## Kiswahili na Vijana

**Zawadi Sakapalla**

SakapallaCC@gmail.com

Lengo la makala hii ni kueleza jinsi Kiswahili kilivyo na nafasi katika kuwajengea vijana hali ya kujitambua, kujiamini, na kuendeleza utamaduni wetu, hasa kwa watoto wanaokulia nje ya Tanzania. Makala inatoa mifano halisi kutoka katika kazi kama vile *Let's Go Volunteer, Twende Tukajitolee* na vitabu vya kuchora. Makala inadhihirisha kuwa, kupitia vitabu hivyo, Kiswahili kinaweza kuimarisha uhusiano wa kifamilia, kijamii, na kitaifa, hasa watoto wa diaspora wanapoweza kuwasiliana na ndugu bila vikwazo. Zaidi, makala inatoa mifano ya jinsi Kiswahili kinavyotumika katika programu za maendeleo ya vijana kupitia hadithi za kiutamaduni, mafunzo ya elimu ya fedha, na programu za kujitolea. Programu hizi huwapa vijana nafasi ya kutumia Kiswahili katika mazingira halisi huku wakijielimisha, kubadilishana utamaduni, na kushiriki katika miradi ya maendeleo ya jamii. Makala pia inaonesha kwa mifano kuhusu vijana wa diaspora ya Kitanzania walioshiriki programu hizi na baadaye kukubaliwa katika vyuo vikuu kama Harvard, Yale, Columbia, na Duke. Mafanikio yao yanaonyesha kuwa misingi ya utamaduni, uongozi, kujitolea, na kujiamini kwa lugha mbili huimarisha ubora wa kitaaluma.

# Mchango wa Riwaya ya Kiswahili katika Kufundisha Diplomasia: Mfano wa Riwaya ya *Kusadikika*

**Athumani S. Ponera**
atponeraman@gmail.com

Makala hii inajadili namna mwandishi wa riwaya ya *Kusadikika* anavyoifunza jamii kuhusu misingi, aina, na umuhimu wa diplomasia katika kuistawisha jamii. Utafiti uliozaa makala hii ulifanyika maktabani, huku ukijiegemeza katika mkabala wa kitaamuli. Ikitumia Nadharia ya Uhemenitiki, makala inabainisha kuwa riwaya ya *Kusadikika* imeakisi aina, misingi, na umuhimu wa diplomasia katika kuendeleza jamii. Kuhusu aina, riwaya imetumia *diplomasia ya kibalozi* kupitia wajumbe sita waliotumwa katika nchi zote zinazopakana na nchi ya Kusadikika. Riwaya inahimiza misingi ifuatayo ya kidiplomasia ili kupata ustawi: Kusadikika ishirikiane na nchi nyingine; yafanyike majadiliano ili kuijenga Kusadikika; kuthamini utu wa wana-Kusadikika wote; Kusadikika iwe na ustawi unaolandana na nchi jirani; kila mwana-Kusadikika awajibike katika kuijenga nchi; na kila mwana-Kusadikika awe mwadilifu. Riwaya inaonesha kuwa diplomasia husaidia: kuushikamanisha ulimwengu; kudumisha amani ulimwenguni; na kulinganishia ustawi wa jamii katika nyanja mbalimbali. Makala inahitimisha kuwa riwaya teule ina maudhui faafu katika kufundisha diplomasia; hivyo haina budi kuendelea kufundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu.

# Ukiona Vyaelea Vimeundwa: Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani

**Mussa. M. Hans**

hansmussa@udsm.ac.tz/ mussahans30@gmail.com

Ni vigumu sana kutaja maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Bara la Afrika bila kuitaja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kuanzia sasa, Tanzania). Tanzania ni nchi pekee duniani yenye mabaraza mawili ya Kiswahili. Pia, Tanzania ina vyuo vikuu viwili (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar) ambapo kila Chuo kina Idara mbili zinazosimamia utafiti na ufundishaji katika lugha ya Kiswahili. Aidha, nchi ya Tanzania ina sera, mipango, na mikakati mbalimbali inayohusu lugha ya Kiswahili. Jitihada hizi za kitaifa zilianza hata kabla ya kupata uhuru. Mathalani, mwaka 1954 chama cha TANU kilitangaza rasmi kwamba Kiswahili kitakuwa lugha ya ukombozi. Msingi huo wa Kiswahili kuteuliwa na TANU kuwa lugha ya ukombozi, hatimaye umekuja kuzingatiwa katika uamuzi wa kukipa hadhi Kiswahili kuwa na siku yake maalum duniani. Lengo la makala hii ni kujadili mchango wa Tanzania katika maendeleo ya Kiswahili ulimwenguni na, hatimaye, kujenga utangamano wa kitaifa na kimataifa. Data za utafiti uliozaa makala hii zimepatikana kwa njia mbili, upitiaji wa nyaraka za maktabani na usaili. Makala inaanza kwa kubainisha historia ya maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania, jitihada zilizofanyika, na zinazoendelea kufanyika. Pia, inabainisha changamoto na namna ya kuzitatua.

# Ufanisi wa Kiswahili katika Kujenga Umoja na Maendeleo Madhubuti ya Afrika Kupitia Teknolojia ya Akili Unde (AU)

**Aldin Mutembei**
kaimutembei@gmail.com

Makala hii inafafanua jukumu la kimkakati la Kiswahili kama lugha ya mawasiliano katika kukuza umoja wa Kiafrika na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika muktadha wa teknolojia za AkiliUnde (AU). Kwa kuzingatia nadharia za lugha na maendeleo, utafiti uliozaa makala hii unasisitiza kwamba kufundisha na kujifunza Kiswahili kupitia lugha nyingine za asili za Afrika kutaongeza ushirikishwaji, uelewekaji na kujiona wamoja; hivyo kuimarisha mshikamano na Umoja wa Afrika. Aidha, makala inajadili kuwa matumizi ya teknolojia ya AU katika elimu ya lugha na lugha ya Kiswahili yanatoa fursa mpya katika ujuzi wa uhifadhi wa lugha za asili, mawasiliano ya kitamaduni, na kuchochea uvumbuzi wa kiteknolojia. Kupitia uchambuzi wa machapisho yanayohusu elimu ya lugha mbalimbali za Afrika, sera za lugha barani Afrika, na teknolojia za AU katika lugha, makala hii inadhihirisha kwamba Kiswahili kinaweza kutumika kama nyenzo ya umoja wa kitamaduni na maendeleo ya kiuchumi na kijamii endapo kitaungwa mkono na suluhisho za AU zinazoheshimu ikolojia ya lugha za asili za Afrika.

**Dhana za msingi**: Teknolojia za AU, nadharia ya lugha na maendeleo, sera, ikolojia


# Mdhihiriko wa Mitindo ya Lugha katika Hotuba za Rais Dkt. Mwinyi katika Kuhimiza Amani, Mshikamano na Maendeleo

**Riziki Pembe Juma & Ahmad Yahya Sovu**

*rikikijamal@yahoo.com* & *sovu82@gmail.com*

Makala hii inafafanua namna mitindo ya lugha inayodhihirika katika hotuba za Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar, katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2025 na inavyohimiza amani, mshikamano na maendeleo. Data za makala zilikusanywa kwa kutumia mbinu kuu tatu: mahojiano, hojaji, na udurusu wa maktabani. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Ushawishi. Matokeo yamedhihirisha kuwa katika hotuba zake, Mhe. Rais Mwinyi hutumia mitindo ifuatayo ya lugha: takwimu, ucheshi, tafsida, misemo, majazi, tashbiha, takriri, masimulizi ya hadithi na kuchanganya msimbo. Pia, imebainika kuwa mitindo hiyo hutumika kama zana za kutuliza misuguano, kuhimiza maridhiano na kuwaleta wananchi pamoja katika ajenda za maendeleo. Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mitindo katika hotuba za Mhe. Rais Mwinyi si mapambo ya lugha pekee, bali ni mbinu mahsusi za kujenga fikra shirikishi, kuendeleza amani na kuimarisha mshikamano wa kijamii visiwani Zanzibar.

**Maneno Muhimu**: Mitindo, Amani, mshikamano



"Kukataa kabila lako ni ubaguzi, lakini kukataa lugha yako ni kujiuza. Lugha ya Kiswahili ni utambulisho wetu na nguzo ya umoja wetu kama Watanzania."

**Baba wa Taifa, Mwl. Julius K Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO